

APRM TANZANIA

Shiriki • Toa Maoni • Chochea Maendeleo

www.aprmtanzania.or.tz

APRM ni nini?

APRM (African Peer Review Mechanism) ni Mpango wa hiari wa Nchi za Afrika wa Kujitathmini kwa vigezo vya Utawala Bora, ulioanzishwa mwaka 2003 ili kuziwezesha nchi za Afrika kujitathmini, kubaini maeneo yaliyofanya vizuri, changamoto zilizojitokeza na kuweka mikakati ya kuzitatua kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kimataifa kuhusu Utawala Bora.

Katika jitihada za Bara la Afrika kujenga misingi imara ya utawala bora, kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kuimarisha ustawi wa jamii. Mwaka 2002, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika walitoa Tamko la Mpango Mpya wa Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika (NEPAD), lililoweka msisitizo katika kuimarisha masuala ya demokrasia, siasa, uchumi na utawala wa mashirika ya biashara.

Kimsingi, kuanzishwa kwa APRM kulizingatia matokeo ya tafiti za kitaalamu zilizobainisha uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya ustawi wa Utawala Bora na ukuaji wa uchumi, ambapo dhana hiyo imeendelea kutambuliwa kama kichocheo kikuu cha uwekezaji na ushindani wa nchi katika masoko ya dunia.

MISINGI YA APRM TANZANIA

Shughuli za APRM zinatekelezwa kwa kuzingatia misingi mikuu mitatu:



KWA NINI APRM NI MUHIMU?

APRM ni muhimu kwa kuwa hutoa fursa kwa nchi kujitathmini, kubaini maeneo yaliyofanya vizuri na kuyaendeleza pamoja na kuainisha changamoto zilizojitokeza na kuweka mikakati ya kuzitatua.

Kupitia tathmini hizo, nchi yetu hupata fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu na nchi nyingine, jambo linalochangia kuimarisha sera, sheria, taasisi na mifumo ya utawala kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

MAJUKUMU YA APRM

Moja ya jukumu la msingi la APRM Tanzania ni kufanya Tathmini katika maeneo yafuatayo :



Majukumu ya ziada ni pamoja na;

- Kutoa tahadhari ya awali katika kuzuia migogoro na kuimarisha Amani.
- Kuzisaidia na kuziwezesha nchi za Afrika katika utayarishaji wa Ripoti za Uwezo wa Nchi Kukopesheka Kimataifa (International Credit Rating).
- Kutayarisha Ripoti ya Utawala Bora ya Afrika (African Governance Index).
- Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika na Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu (SDGs).

MANUFAA YA TATHMINI ZA APRM TANZANIA

• Ripoti za APRM zimeendelea kutumika kama rejea muhimu juu ya masuala ya Utawala Bora ndani na nje ya Nchi.

• Mpango huu unagusa maslahi ya Wananchi walio wengi. Hivyo, umesaidia kutimiza dhana inayoungwa mkono duniani kote ya utawala shirikishi unaowapa wananchi fursa ya kuishauri Serikali yao.

• Mpango huu pia umelipatia Taifa letu nafasi ya kujikosoa kwa kutumia wataalamu wake wa ndani na hivyo kujenga uwezo na kuongeza idadi ya wataalamu hao kwa kuhakikisha kuwa maarifa yao yanatumika ili kuleta ufanisi katika kukuza uchumi.

• Mpango huu pia umekuwa fursa adhimu kwa Serikali kuweza kupata mrejesho juu ya sera, sheria na mikakati mingine ambayo Serikali inaitekeleza. Taasisi ya APRM imekuwa kiungo kinachofanya tafiti na kubaini penye mazuri na kuongeza nuru na penye udhaifu wa kufanyiwa kazi.

• APRM imeipa nchi yetu fursa ya kuwaonesha kwa uwazi zaidi wabia wetu wa maendeleo na wawekezaji jitihada zetu za kujikwamua kiuchumi na kijamii na mikakati ya kuimarisha utawala bora. Hivyo, kuwapa imani na kuvutia uwekezaji zaidi na kuendeleza heshima ya nchi yetu katika uso wa kimataifa.

MATOKEO YA TATHMINI ZA APRM TANZANIA

Shughuli za APRM Tanzania zimeendelea kutoa taarifa muhimu ambazo zimetumika katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo ya Taifa. Hadi sasa Serikali ya Tanzania imeweza kupata mafanikio yafuatayo:



• Kuanzishwa kwa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ;

• Maboresho ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki (EFDs) ;

• Kuanzishwa kwa National Financial Crisis Management Plan ;

• Kuanzishwa kwa taasisi ikiwemo ZAECA, ZURA na ZPRA ;

• Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ;

• Kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa Wahitaji ya mwaka 2017 ;

• Maboresho katika elimu, miundombinu na huduma za jamii ;

• Kuimarika kwa mifumo ya utawala na usimamizi wa rasilimali za Taifa.

APRM KATIKA SHUGHULI ZA SERIKALI NA KWA WANANCHI

APRM ni kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi katika mchakato wa maendeleo, kwa kuisaidia Serikali kupata mrejesho kuhusu utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ili kuimarisha mafanikio na kuboresha maeneo yanayohitaji hatua zaidi.

Kwa upande wa Serikali, APRM hutoa fursa ya kujitathmini na kuainisha hatua, jitihada na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Aidha, kupitia jukwaa hili, Tanzania huwasilisha kwa jamii ya kitaifa na kimataifa simulizi yake yenyewe kuhusu maendeleo na juhudi zake za kuimarisha utawala bora kwa ustawi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa upande wa wananchi, APRM hutoa fursa ya kushiriki katika kupanga shughuli za maendeleo yao, kutoa maoni na mrejesho kuhusu sera, mipango na mikakati ya maendeleo. Ushiriki huu huimarisha dhana ya utawala shirikishi na uwajibikaji wa viongozi kwa Wananchi wao.

Dhana ya APRM ya kujitathmini na kujisahihisha inajengwa juu ya misingi ya ushirikishwaji wa wananchi iliyosisitizwa na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kitabu chake cha "***Tujisahihishe***" (1962), aliposema:

"Hatuna budi kuona daima kwamba mambo tunayoyazungumza yanatokana na watu, au mawazo yetu yanakubaliwa na watu."



SHIRIKI APRM

Ushiriki wako katika shughuli za APRM Tanzania ni msingi muhimu wa kujenga Taifa lenye utawala bora, uwajibikaji na maendeleo endelevu.

Sauti yako ina thamani. Shiriki APRM kwa maendeleo ya Taifa na ustawi wa jamii.

Wasiliana nasi kupitia:
APRM Tanzania
Ghorofa ya 3, Jengo la JNICC
S.L.P 8315
Dar es Salaam
Website: www.aprmtanzania.or.tz
Email: info@aprmtanzania.or.tz
or aprm@aprmtanzania.or.tz